# LISHE UPDATES

Imetolewa na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania

TOLEO No. 004 JULAI 01, 2025


## MAFANIKIO, MIKAKATI YA TFNC KWA MWAKA 2025/26

Na Mwandishi Wetu, Dar es Salaam



Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) ni taasisi ya umma chini ya Wizara ya Afya iliyoanzishwa mwaka 1973 kwa Sheria ya Bunge Sura 109. Dhumuni kuu la kuanzishwa kwa Taasisi hii ni kuwa na mfumo madhubuti wa kitaasisi utakaounganisha Serikali kuongoza harakati za kitaifa katika mapambano dhidi ya aina zote za utapiamlo nchini. Tokea kuanzishwa kwa Taasisi, mrengo wa kupambana na changamoto za lishe duni zimebadilika kutoka kuweka msisitizo katika upatikanaji wa chakula (food security); kwenda tiba za utapiamlo hadi sasa ambapo msisitizo mkubwa ni katika kuzuia visababishi vya utapiamlo katika ngazi zote yaani mtu binafsi, kaya na jamii na mazingira wezeshi (ambapo hapa hujumuisha sera, miongozo nk.).

Habari inaendelea ukurasa wa 2...

## Bunge lapitisha Trilioni 1.68 bajeti ya Wizara ya Afya 2025/26




Waziri wa Afya, Mhe. Jenister Mhagama (MB), akionesha begi la Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/26 wakati akielekea kuiwasilisha Bungeni.

Na Hamza Mwangomale, Dar es salaam.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lapitisha Shilingi Trilioni 1.68 ikiwa ni makadilio ya Bajeti ya Wizara ya Afya kwa ajili ya kutumika kutekeleza vipaumbele na afua mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2025/26.

Akiwasilisha bajeti hiyo, Bungeni jijini Dodoma Juni 02, 2025 Waziri wa Afya, Mhe. Jenista Mhagama amesema kuwa Wizara ya Afya itaimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ikiwemo magonjwa ya kuambukiza, magonjwa ya milipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, magonjwa yasiyoambukiza na huduma za lishe kwa kutekeleza afua mbalimbali.

“Tutaimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga kwa kutekeleza afua ikijumuisha ununuzi na usambazaji wa dawa muhimu za uzazi salama pamoja na dawa za uzazi wa mpango, dawa kinga za minyoo, dawa za kuongeza damu, dawa za malaria, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi,” amesema Waziri Mhagama.

Aidaha, Waziri Mhagama amesema kuwa katika kipindi kijacho Wizara itajielekeza katika kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwepo kutenga fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya Sera za Kimataifa na ufadhili wa Sekta ya Afya.

Awali akisoma taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/25, Waziri Mhagama amesema wizara imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo uboreshaji wa hali ya lishe nchini kulikochangiwa na utekelezaji wa afua mbalimbali za afya na lishe.

“Lishe bora ni muhimu kwa uhai, ukuaji na maendeleo ya binadamu kiakili na kimwili na hivyo huchangia katika kuongeza tija katika uzalishaji mali kwa kaya na kuimarisha uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Habari inaendelea ukurasa wa 2.

# PANITA, TFNC zawajengea uwezo waandishi wa habari

Na Hamza Mwangomale, Dar es salaam.

Jukwaa la Lishe Tanzania (PANITA) na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) wamendesha semina ya siku moja kwa waandishi wa habari inayolenga kuwaongeza uelewa wa mambo mbalimbali ya lishe ikiwemo michakato ya "Nutritionfor Growth", hali ya lishe nchini, mipango ya Serikali, na jukumu la vyombo vya habari katika kuboresha lishe na kuongeza uelewa wa umma juu ya masuala ya lishe.

Akiongea wakati wa kufungua semina hiyo Mkurugenzi wa PANITA, Tumaini Mikindo amesema kuwa waandishi wa habari ni nguzo muhimu katika kuufikia umma. "Masuala ya lishe ni mtambuka, yanahitaji jitihada ya sekta mbalimbali ndio maana zamani wakati suala hili lilihusisha sekta ya afya pekee matatizo ya lishe yalikuwa yanadhibitiwa na kujirudia mara kwa mara, mfano mkoa wa Iringa katika miaka ya tisini, Serikali ilitangaza kutokomeza kabisa tatizo la udumavu, lakini baada ya muda tatizo hilo lilirudi kwa kasi kubwa. Hivyo tunatami kuona kila mmoja anashiriki mapambano dhidi ya aina zote ya utapiamlo, na kama vyombo vya habari vitasemea kwa usahihi taarifa za lishe, jambo hili litawezekana. " Amesema Mikindo.

Akiwasilisha mada wakati wa semina hiyo, Afisa Mtafiti wa Sera na Mipango ya Lishe kutoka TFNC, Geofrey Chiduo amesema kuwa sasa Tanzania kumekuwa na ongezeko kubwa la kusambaa taarifa zisizo sahihi za masuala ya lishe, huku waandishi wa habari wakiwa ni sehemu moja wapo ya kusambaza taarifa hizo, jambo linalotishia usalama wa afya na lishe ya jamii.

Chiduo amesema kuwa lishe bora ni msingi wa maendeleo kwani mtu akiwa na lishe bora afya yake huimarika na hivyo kuweza kufanya kazi kwa tija. Hivyo ametoa rai kwa waandishi wa habari nchini kuhakikisha wanaongeza umakini na kuzuia upotoshaji wa taarifa za lishe.

"Ni vyema mwandishi wa habari wakawa na uelewa sahihi wa jambo analoripoti ili

Habari hii inaendelea kurasa ya 04.

# MAFANIKIO, MIKAKATI YA TFNC KWA MWAKA 2025/26

inaendelea kutoka kurasa ya 01.

Kwa ujumla mafanikio makubwa yamepatikana tangu kuanzishwa kwa mfumo rasmi wa kupambana na changamoto za utapiamlo, ikiwemo kupunguza viwango vya utapiamlo kwa makundi yanayotiwa msisitizo. Udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano umepungua kutoka 34% mwaka 2015/16 hadi 30% mwaka 2022; ukondefu kutoka 5% hadi 3.5%, uzito pungufu kutoka 14% hadi 12% na uzito mdogo wa kuzaliwa (chini ya kg 2.5) kutoka 12% hadi 6%. Kupungua kwa viashiria hivi umechangia kupungua kwa vifo vya watoto chini ya miaka mitano (5) kutoka 67 hadi 43 kwa vizazi hai 1,000 na vifo vya watoto wachanga kutoka 43 hadi 33 kwa vizazi hai 1,000.

Mafanikio haya ni matokeo ya jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kupitia TFNC, ambapo kwa mwaka 2024/2025 Taasisi inajivunia kutekeleza mambo yafuatayo:

Kupitishwa kwa Kanuni za urutibishaji wa vyakula vinavyosindikwa (Food Fortification Regulations) ambapo kwa sasa kibebeo cha chumvi kimejumuishwa katika kanuni hii. Hii inaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza katika nchi za ukanda wa kusini mwa jangwa la Sahara (SADC) kupitisha kanuni zenye majumuisho hayo.

Kwa upande wa tafiti, Taasisi imefanikiwa kufanya tafiti kubwa tano (5) za kimkakati ikiwemo utafiti wa Gharama za Utapiamlo (The Cost of Hunger Study (COHA)); utafiti wa Majaribio ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa Matumizi ya Chumvi yenye Madinijoto unaofanyika katika Mikoa ya Dar Es Salaam, Mtwara na Singida (FORTMAS); utafiti wa kuimarisha hali ya lishe na afya ya mama na vijana (IMAN); utafiti wa kutengeneza asusa yenye madini chuma kwa wingi (Bright Future Snack Bar) kwa kushirikiana na wajasiriamali wa ndani ya nchi pamoja na utafiti wa kutengeneza uji unaotokana na mbegu za mchicha (AMARANTH).

Aidha kwa upande wa kutoa elimu ya lishe kwa umma katika kipindi hiki cha mwaka 2024/25 Taasisi imefanikiwa kuendesha kozi tano (5) za muda mfupi na kufanikiwa kufikia jumla ya washiriki 358 ambayo ni nyongeza ya asimilia 99 ya lengo la kufikia washiriki 180. Aidha, sambaba na hilo Taasisi imeandaa na kurusha jumla ya vipindi 78 kwa njia ya runinga na redio, na kurusha jumla ya jumbe 326 katika mitandao ya kijamii ambayo kwa pamoja imefikia takribani watu million saba (7) kati ya 15 waliolengwa kufikiwa.

Kwa upande wa huduma za maabara, Taasisi imeendelea kupokea sampuli kutoka nchi mbalimbali za ndani na nje ya bara la Afrika hadi kufikia nchi 16 (kutoka 11). Kwa mwaka wa fedha 2024/25, maabara imepokea sampuli 6000 kutoka Kenya na Ethiopia. Aidha, sampuli nyingine 6000 zilikuwa zipokelewe kutoka Malawi lakini kutokana na kuchelewa kukamilika kwa DHS ya nchi hiyo, sampuli hizo sasa zitapokelewa na kufanyiwa uchambuzi katika mwaka wa fedha 2025/26. Jambo muhimu la kukumbuka ni kwamba mwaka 2023 maabara ya TFNC ilitambuliwa kama maabara ya rejea ya masuala ya chakula na lishe na wanachama wa ECSA-HC na IGAD.

Pia Taasisi imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuratibu masuala ya lishe nchini ambapo jumla ya vikao vya kitaalamu 13 ikiwemo vikao 3 vya juu vya Makatibu Wakuu vimefanyika. Mkutano wa mwaka wa masuala ya lishe ulifanyika Mwanza na jumla ya wadau 380 walishiriki. Taasisi inaendelea kusimamia mapitio ya kati ya Mpango Jumuishi wa Kisekta wa Lishe (NMNAP II) ambapo kwa sasa timu inakusanya taarifa katika ngazi mbalimbali. Aidha, Tanzania imewasilisha maazimio sita (6) katika jukwaa la Lishe kwa Maendeleo (Nutrition for Growth Summit (N4G)). Tanzania ni miongoni mwa nchi 60 waliopitisha "endorse" mkataba wa kidunia wa masuala ya lishe (Global Nutrition Integration Compact). Aidha Taasisi imeteuliwa kuwa mratibu wa Vuguvugu la Lishe (Scaling Up Nutrition (SUN) Movement Focal Person) kwa Tanzania.

### Maeneo ya Kimkakati kwa mwaka 2025/26

1. PROGRAMU ZA KITAIFA:
   Taasisi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Ofisi ya Raisi – TAMISEMI, na wadau wa maendeleo inatarajia kuandaa na

Habari inaendelea ukurasa wa 3...

# MAFANIKIO, MIKAKATI YA TFNC 2025/26



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akionesha tuzo maalumu ya "The Global Goalkeeper Award" aliyotunukiwa na Taasisi ya Gates Foundations ya Marekani Februari 4, 2025 jijini Dar es Salaam

inaendelea kutoka kurasa ya 02

**Maeneo ya Kimkakati kwa mwaka 2025/26**

1. kusimamia maandalizi ya uhamaji kutoka matumizi ya vidonge vya madinichuma na aside ya foliki (IFAS/FEFO) kwenda vidonge mseto (Multiple Micronutrient Supplements). Mabadiliko haya yanatokana na mafanikio ya mradi wa IMAN yaliyoonesha kukubalika zaidi kwa aina hii ya vidonge kwa wajawazito; na uwezo wa mfumo wa afya na mnyororo wa bidhaa kuweza kuhimili mabadiliko haya. Pia, mabadiliko haya yatachagiza kupunguza matokeo hasi kwa wanawake wanaojifungua na watoto kama vile watoto kuzaliwa na uzito mdogo (LBW), kuzaliwa kabla ya wakati (prematurity) na vifo kwa watoto wachanga (neonatal death).

2. UTAFITI:
   Taasisi imepanga kutekeleza tafiti kubwa nne (4) za kimkakati ambazo ni 1) Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya taarifa za lishe (Nutrition Surveillance System); 2) Kupanua wigo wa mradi wa FORTMAS; 3) Majaribio ya mfumo wa kuingia ubia na wajasiriamali kwa bidhaa zitakazokuwa zinazalishwa na Taasisi na 4) Kukamilisha mradi wa utengenezaji wa uji unaotokana na mchicha (AMARANTH). mwilini.

2. ELIMU YA LISHE KWA UMMA:
   Kuongeza idadi ya kozi fupi zinazotolewa na Taasisi kutoka tano (5) kufikia nane (8) na kuongeza idadi ya washiriki hadi 800. Pia, kuongeza idadi ya vipindi vya masuala ya lishe vinavyotolewa kupitia runinga na redio kufikia 100 na jumbe za lishe kupitia mitandao ya kijamii kufikia 600 kwa lengo la kufikia wasikilizaji million 15. Aidha, Taasisi inalengo la kuendelea kupanua wigo wa vyanzo vya elimu na taarifa za lishe kwa watu wenye mahitaji maalum kwa kusambaza vitabu vya maandishi ya nukta nundu pamoja na viredio vyenye taarifa na jumbe zilizorekodiwa kwa kundi la watu wasioona, pamoja na kuendelea kufanya maboresho kwenye aplikesheni ya kimtandao (Lishe App) ili iweze kupakuliwa na simu zenye kutumia mfumo wa "ios". Maboresho haya yanatarajiwa kuwezesha kufikia watu takribani million 10 kutoka milioni 4 wa sasa wanaotumia simu janja (smart phone).

3. MAABARA:
   Kuanza maombi ya kupata ithibati ya maabara kutoka "SaDiQAS" baada ya kukamilika kwa miongozi ya ndani, mafunzo kwa watumishi pamoja na uboreshaji wa mazingira ya kazi. Kuongeza idadi ya huduma za uchambuzi wa kimaabara zinazotolewa kujumuisha vipimo vya kitiba pamoja na kuongeza idadi ya sampuli zinazopokelewa na Taasisi kufikia 10,000 kwa mwaka.

4. KUIMARISHA URATIBU WA MASUALA YA LISHE KWA KUSHIRIKIANA NA OFISI YA WAZIRI MKUU:
   Taasisi imepanga kuanza maandalizi ya uandaaji wa Mpango Jumuishi wa tatu wa utekelezaji wa masuala ya lishe wa miaka mitano (3rd National Multisectoral Nutrition Action Plan – 2026/27 – 2030/31) ili kutoa mwongozo kwa wadau wote kuhusu utelelezaji wa afua za lishe. Kuendelea kujenga uwezo wa kisekta kujumuisha masuala ya lishe katika mipango yao na kuimarisha ukusanyaji wa fedha kwa ajili ya afua za lishe ikiwemo kutambua vyanzo vipya vya ufadhili wa masuala ya lishe. Aidha, Taasisi inalenga kuanzisha utaratibu wa kujinadi nje ya nchi kwa kazi za kisayansi (consultancy) na maabara yake kwa upana zaidi.



# PANITA, TFNZ zawajengea uwezo waandishi wa habari



Mtafiti wa Sera na Mipango ya Lishe TFNC, Geofrey Chidua akiwasilisha mada wakati wa mafunzo ya ya waandishi wa habari yaliyoandaliwa na PANITA kwa kushirikiana na TFNC

inaendelea kutoka kurasa ya 02.

kuzuia upotoshaji. Mfano kunachombo kimoja walikuwa wanamuhoji msanii wa kike ambaye alikuwa anajisifu kwamba amemnyonyesha mwanaye kwa muda wa wiki mbili tu na kumuachisha ziwa, bila ya mtoto huyo kupata madhara yoyote ya kiafya. Mtangazaji aliyekuwa anafanya mahojiano hayo kama angekuwa na uelewa sahihi wa masuala ya lishe, angeweza kumrekebisha msanii huyo, na kumuwezesha mtazamaji kupata ujumbe sahihi yuu ya umuhimu wa kumnyonyesha mtoto maziwa ya mama" Amesema Chiduo.

Akitoa neno la shukrani kwa PANITA na TFNC Mhariri wa Press Media, Neville Meena amesema kuwa mafunzo waliyoyapata katika semina hiyo yamewajenga sana wao binafsi kama waandishi wa habari kwa kutambua umuhimu wa lishe katika maisha ya kila siku. Pia amesema kuwa hii itasaidia kuongeza hari za waandishi wa habari kuripoti zaidi taarifa za lishe kwani kwa sasa masula ya lishe hayapewi sana kipaumbele katika vyombo vingi vya habari.

"Tunaomba PANITA na TFNC waendelee kutupatia mafunzo ya namna hii mara kwa mara kwani itasaidia kutufanya kuwa wabobezi katika kuandika na kuripoti taarifa za lishe, kwa mfano tunaenda bungeni kuripoti bajeti za wizara mbalimbali. Hivyo kupitia mafunzo haya sisi kama waandishi wa habari tunaweza kujiuliza ni kwa namna gani bajeti hizo zimegusia masuala ya lishe, ikizingatiwa kuwa lishe ni sekta mtambuka" amesema Meena.

# Wadau, Wataalamu wa usindikaji wanolewa

Na Jackson Monela, Morogoro.

Serikali imetoa mafunzo kwa wadau na wataalamu wa urutubishaji wa vyakula nchini kwa ajili ya kuwajengea uwezo na uelewa juu ya sharia na kanuni za usindikaji Tanzania zilizozinduliwa rasmi Aprili 2024.

Akiongea wakati wa kufungua mafunzo hayo kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Afisa Biashara Mwandamizi Festo Kapela amesema kuwa dhamira ya serikali ni kuona watanzania wanapata vyakula ambavyo vina ubora kilishe lakini vyenye virutubishi muhimu kwa ustawi wa afya zao.

"kabla sheria na kanuni hizi wazalishaji wa vyakula kulikuwa na kulaumiana ya kwamba baadhi walikuwa wakiwema virutubishi lakini wengine hawaweki na kulifanya jambo kuwa ngumu katika utekelezaji wake "amesema Kapela

Aidha Kapela amesema kuwa lishe inamchango mkubwa katika maendeleo ya taifa kwani mbali na kuimarisha hali ya afya na lishe ya mtu mmoja mmoja, lakini pia lishe ni muhimuli katika kuzalisha nguvu kazi yenye tija na kutoa mchango chanya katika maendeleo ya kiuchumi, hivyo ameziomba sekta binafsi zinazojihusisha na uzalishaji wa vyakula kutekeleza suala hilo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), Mkurugenzi wa Idara ya Afya na Lishe ya Jamii, Dkt. Ray Masumo amesema kuwa TFNC imekuwa na mchango mkubwa katika kuanzisha, kuendeleza na kukuza ushiriki wa wadau mbalimbali katika utekelezaji wa afua za uongezwaji wa virutubishi kwenye vyakula.

Akiwasilisha salamu za wadau wa maendeleo mtaalamu wa lishe Bi Joyce Ngegba kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF), ambaye pia amemwakilisha Msimamizi Mkuu wa Shule za nchini kutoka shirika hilo, ameeleza namna shirika lilivyo msatari wa mbele katika kufadhili na kuendeleza utekelezaji wa afua za uongezwaji wa virutubishi kwenye chakula.

Mafunzo hayo ya siku nne yaliyofanyika mkoani Morogoro yameandaliwa na Jukwaa la Wadau wa Uongezaji Virutubishi kwenye vyakula nchini (The Tanzania Food Fortification Alliance) (TFFA), Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Afya, Taasisi ya Food Fortification Initiative (FFI), Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania chini ya uwezeshaji kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF).

# Bunge lapitisha Trilioni 1.68 bajeti ya Wizara ya Afya 2025/26

inaendelea kutoka kurasa ya 01.

Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa pili wa Kitaifa wa Lishe (National Multisectoral Nutrition Action Plan (2021/22 -2025/26)" amesema Waziri Mhagama.

Waziri Mhagama, ameongeza kuwa kupitia Mpango huo Wizara imekuwa ikitekeleza afua za lishe zilizothibishwa kuwa na matokeo makubwa katika kukabiliana na matatizo ya utapiamlo nchini ikiwemo matatizo ya lishe duni, lishe ya kuzidi na upungufu wa vitamini na madini mwilini. Waziri Mhagama ametaja baadhi ya afua hizo kuwa ni pamoja na utoaji wa matone ya Vitamini A, kinga na matibabu ya utapiamlo mkali, uongezwaji wa virutubishi vya madini na vitamini kwenye vyakula na utoaji wa elimu ya lishe kwa umma.

# Wafanyakazi TAWLA wapatiwa semina ya Ulaji na TFNC




Afisa Lishe Mwandamizi kutoka TFNC akiwasilisha mada ya ulaji na mitindo bora ya maisha kwa wafanyakazi wa TAWLA kwa njia ya mtandao

Na Hamza Mwangomale, Dar es Salaam

Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) imetoa semina ya ulaji na mitindo bora ya maisha ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza kwa wafanyakazi wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA).

Akitoa semina hiyo kupitia mkutano mtandao (zoom meeting), Afisa Lishe Mwandamini kutoka TFNC, Adeline Munuo amesema kuwa lengo la semina hiyo ni kuwawezesha watumishi wa TAWLA kuelewa na kuzingatia ulaji bora na mtindo mzuri wa maisha ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.

"Kupitia semina hii, tumeweza kuwaeleza wafanyakazi wa TAWLA dhana ya magonjwa yasiyombukiza, tabia hatarishi zinazochangia kuongezeka kwa magonjwa hayo na namna ya kujikinga kupitia ulaji unaofaa na mitindo bora ya maisha" amesema Munuo.

Munuo ametaja njia mbalimbali za kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo; kutumia vyakula vya asili zaidi kama vile nafaka zisizokobolewa, kula mbogamboga na matunda kila siku angalau aina tano, kupunguza vyakula vilivyosindikwa (high processed foods) kama vile soseji, biskuti na vinjwaji vyenye sukari. Njia nyingine alizozitaja ni kupunguza matumizi ya vyakula vyenye sukari, mafuta na chumvi kwa wingi pamoja na kufuatilia uzito na mzunguko wa kiuno mara kwa mara. Aidha Munuo amesema kuwa ulaji unaofaa na mitindo bora ya maisha ni kinga bora ya magonjwa yasiyoambukiza kama vile kisukari, maonjwa ya moyo na baadhi ya saratani ambayo yamekuwa na gharama kubwa katika kuyatibu, na kudhohofisha nguvu kazi. Hivyo ametoa wito kwa taasisi mbalimbali kujiwekea utaratibu wa kuwapia semina za namna hiyo watumishi wake kwani ili kuimarisha afya zao na kuwa na uhakika wa nguvu kazi yenye tija.

Kwa upande wake Afisa Sheria wa TAWLA, Yosia Kimweri ameishukuru TFNC kwa kuwapatia semina hiyo ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha ustawi wa rasilimali yenye tija na endelevu katika kufikia malengo ya taasisi yao.

"Sasa hivi kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa yasiyoambukiza ambayo yanachangia kufifisha uwezo wa nguvu kazi kufanya kazi kwa tija. Hivyo kupitia semina hii tuliyopewa na wataalamu kutoka TFNC tunaamini kuwa itatusaidia mtu mmoja mmoja na Taasisi kwa ujumla kuwa na wafanyakazi wenye afya njema" Amsema Kimweri.

# Wadau, wataalamu wa usindikaji wafuliwa

Na Jackson Monela, Dar es salaam

Serikali imetoa mafunzo kwa wadau na wataalamu wa urutubishaji wa vyakula nchini kwa ajili ya kuwajengea uwezo na uelewa juu ya sharia na kanuni za usindikaji Tanzania zilizozinduliwa rasmi Aprili 2024.

Akiongea wakati wa kufungua mafunzo hayo kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Afisa Biashara Mwandamizi Festo Kapela amesema kuwa dhamira ya serikali ni kuona watanzania wanapata vyakula ambavyo vina ubora kilishe.

"kabla sheria na kanuni hizi wazalishaji wa vyakula kulikuwa na kulaumiana ya kwamba baadhi walikuwa wakiwema virutubishi lakini wengine hawaweki na kulifanya jambo kuwa ngumu katika utekelezaji wake "amesema Kapela

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), Mkurugenzi wa Idara ya Afya na Lishe ya Jamii, Dkt. Ray Masumo amesema kuwa TFNC imekuwa na mchango mkubwa katika kuanzisha, kuendeleza na kukuza ushiriki wa wadau mbalimbali katika utekelezaji wa afua za uongezwaji wa virutubishi kwenye vyakula.

Akiwasilisha salamu za wadau wa maendeleo mtaalamu wa lishe Bi Joyce Ngegba kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF), ambaye pia amemwakilisha Msimamizi Mkuu wa Shule za nchini kutoka shirika hilo, ameeleza namna shirika lilivyo msatari wa mbele katika kufadhili na kuendeleza utekelezaji wa afua za uongezwaji wa virutubishi kwenye chakula.

Mafunzo hayo ya siku nne yaliyofanyika mkoani Morogoro yameandaliwa na Jukwaa la Wadau wa Uongezaji Virutubishi kwenye vyakula nchini (The Tanzania Food Fortification Alliance) (TFFA), Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Afya, Taasisi ya Food Fortification Initiative (FFI), Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania chini ya uwezeshaji kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF).

# #TumetekelezaLISHE 2024/2025

**Mafanikio ya LISHE katika sekta mtambuka**

Sauti za MAWAZIRI kutoka BUNGENI

## Wizara ya Mifugo na Uvuvi



**Mhe.Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb.),**
Waziri wa Mifugo na Uvuvi

Serikali imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya mifugo ambapo uzalishaji umeonezeka kama ifuatavyo: Uzalishaji wa nyama umeongezeka **kutoka tani 963,856.55** Mwaka 2023/2024 **hadi tani 1,054,114.03** mwaka 2024/2025.

Uzalishaji wa maziwa umeongezeka **kutoka lita 3,969,887,235.74** mwaka 2023/2024 h**adi kufikia lita 4,009,985,321.20** Mwaka 2024/2025

Aidha katika Sekta ya Uvuvi hadi kufikia Aprili 2025, **jumla ya tani 599,200.33** za mazao ya Uvuvi zilizalishwa **ikilinganishwa na tani 472,579.34** zilizozalishwa katika kipindi kama hiki mwaka 2023/2024. ❞

## Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa



**Mhe. Mohammed O. Mchengerwa (Mb)**
Waziri wa Nchi OR- TAMISEMI

Jumla ya **watoto 7,454,996** wenye umri chini ya miaka mitano wamepimwa hali zao za lishe. Upimaji huo umewezesha kuwabaini na kuwapa matibabu ya utapiamlo mkali **watoto 149,308.** Wazazi na walezi 11,449,738 wamepatiwa elimu na unasihi wa lishe na kuhimizwa kuboresha taratibu za ulishaji wa watoto ili kupunguza udumavu;

**Wajawazito 7,440,632** wamepatiwa vidonge vya kuongeza wingi wa damu ili kukabiliana na tatizo hilo linaochangia vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi. Aidha **watoto 8,944,200** wenye umri chini ya miaka mitano wamepatiwa nyongeza ya matone ya Vitamini A kupitia kampeni za kitaifa zinazofanyika mara mbili kila mwaka ili kuimarisha kinga ya mwili na kupunguza kasi ya maambukizo ya magonjwa yanayochangia tatizo la udumavu; na

Jumla ya **shilingi bilioni 48.56** kutoka mapato ya ndani ya halmashauri (shilingi 1,000 au zaidi kwa kila mtoto chini ya umri wa miaka mitano) zimetolewa na kutumika kutoa huduma katika afua za lishe. Aidha utengaji huo wa fedha kwa kila halmashauri umeimarika kufikia wastani wa kitaifa wa shilingi 1,546. ❞

# #TumetekelezaLISHE 2024/2025

**Mafanikio ya LISHE katika sekta mtambuka**

Sauti za MAWAZIRI kutoka BUNGENI

## Wizara ya Kilimo



**Mhe. Hussein Mohamed Bashe (Mb.)**
Waziri wa Kilimo

ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini na kuondoa utegemezi wa mazao yaliyoongezewa virutubishi kutoka nje ya nchi, hadi kufikia Aprili 2025, Wizara kupitia wataalamu wake **imeweza kuzalisha mbegu mama 250,000 za viazi lishe** sawa **asilimia 71.4** ya lengo la kuzalisha **mbegu 350,000,** uzalishaji unaendelea. Mbegu hizo zimesambazwa katika mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu, Kagera na Mara. Vilevile, wakulima 2,577 wamehamasishwa kuzalisha mazao ya kilimo yenye virutubisho vya lishe yaliyofanyiwa utafiti na wataalam wa hapa nchini. ”



## Wizara ya Viwanda na Biashara

**Mhe.Dkt.Selemani Said Jafo (Mb.)**
Waziri wa Viwanda na Biashara

Katika kutekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe 2021/2022 – 2025/2026, Wizara imefanikiwa kutoa **mafunzo ya kuongeza virutubishi** katika vyakula kwa **wajasiriamali wadogo na wa kati 275** wanaojihusisha na uzalishaji wa unga wa mahindi katika mikoa ya Arusha, Geita, Tanga, Tabora, Kilimanjaro, Simiyu na Shinyanga. Kupitia mafunzo hayo, wajasiriamali wataweza kuzalisha bidhaa zenye ubora unaokidhi soko la ndani na nje ya nchi. ”

# #TumetekelezaLISHE 2024/2025

**Mafanikio ya LISHE katika sekta mtambuka**

Sauti za MAWAZIRI kutoka BUNGENI

## Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia



**Mhe. Prof. Adolf F. Mkenda (Mb.)**

Waziri wa Elimu, Sayansi na

Serikali imewezesha **upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi 15,000** wa vyuo vya maendeleo ya wananchi 54, **wanafunzi 850** wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, wanafunzi 800 wa Chuo cha Ufundi Arusha na **wanafunzi 761** wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya. ❞



## Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

**Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb.)**

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

Wizara imeratibu mafunzo kuhusu **Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto** kwa **Maafisa 281** yanayolenga kuwajengea uwezo katika kusimamia na kuratibu Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM 2021/22 - 2025/26). Aidha, Wizara imetoa mafunzo ya MMMAM kwa **Waandishi wa Habari 26** kutoka katika kila Mkoa ambao ni Vinara katika kutoa taarifa za MMMAM ili kuimarisha utoaji wa elimu ya MMMAM katika jamii. ❞